

**MKATABA WA UWEKEZAJI NA UENDESHAJI WA BUSTANI YA JIJI "CITY PARK"
HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA.**

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 21 ya mwezi Mei Mwaka 2021

KATI YA

HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA, S.L.P 149 Mbeya ambaye kwa madhumuni ya Mkataba huu atajulikana kama **MWAJIRI** kwa upande mmoja.

NA

BABITO TRADING COMPANY LTD, S.L.P 1688 Mbeya ambaye katika mkataba huu atajulikana kama **MWEKEZAJI** kwa upande wa pili.

KWA KUWA mwajiri ameridhia mwekezaji apewe kazi ya uwekezaji na uendeshaji wa Bustani ya Jiji (City park)

KWA KUWA mwekezaji amekubali kuingia mkataba na mwajiri wa kuwekeza na kuendesha Bustani ya Jiji (City park)

KWA HIYO PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA NA KUWEKA MASHARTI YATAKAYOLINDA MAKUBALIANO YA MKATABA HUU KAMA IFUATAVYO:-

1. MUDA WA MKATABA

- i. Mkataba huu utakuwa na muda wa maandalizi wa miezi sita (6) ambapo mwekezaji atatakiwa kujenga miundombinu itakayotumika katika mradi. Muda wa maandalizi utanza kuhesabiwa kuanzia tarehe ya kusainiwa mkataba.
- ii. Mkataba huu utakuwa ni wa miaka kumi (10) kuanzia tarehe 21/05/2021 hadi tarehe 21/05/2031

2 MAHALI PA KAZI

Mwekezaji atawekeza katika eneo la Bustani ya Jiji kiwanja namba 31 kitalu G iliyopo kata ya Sisimba mtaa wa Sokoine Mbeya mjini lenye ukubwa wa Hekta 3.67

3. GHARAMA YA MKATABA

Gharama ya mkataba kwa muda wa uwekezaji wa miaka kumi itakuwa ni Tsh. 563,106,865.65 (Milioni mia tano sitini na tatu mia moja na sita elfu mia nane sitini na tano na senti sitini na tano) kwa mchanganuo ufuatao;

i.	Mwaka wa kwanza	=Tsh.4,000,000.00 x 12 (Miezi) = Tsh. 48,000,000.00
ii.	Mwaka wa pili	= Tsh 4,140,000.00 x 12 (Miezi) = Tsh. 49,680,000.00
iii.	Mwaka wa tatu	= Tsh.4,284,900.00 x 12 (Miezi) = Tsh. 51,418,800.00
iv.	Mwaka wa nne	= Tsh.4,434,871.50 x 12 (Miezi) = Tsh. 53,218,452.00
v.	Mwaka wa tano	= Tsh.4,590,092.00 x 12 (Miezi)= Tsh. 55,081,104.00
vi.	Mwaka wa sita	= Tsh 4,750,745.22 x 12 (Miezi) = Tsh. 57,008,942.64
vii.	Mwaka wa saba	= Tsh.4,917,021.31 x 12 (Miezi) = Tsh. 59,004,255.72
viii.	Mwaka wa nane	= Tsh.5,089,117.05 x 12 (Miezi) = Tsh.61,069,404.60

- ix. Mwaka wa tisa = Tsh.5,267,236.15 x 12 (Miezi) = Tsh.63,206,833.80
- x Mwaka wa kumi =Tsh. 5,451,589.41 x 12 (Miezi) = Tsh. 65,419,072.92

4 TARATIBU ZA MALIPO

- i. Mwekezaji atatakiwa kuweka dhamana ya uwekezaji ya Tsh.12, 000,000.00 (milioni kumi na mbili tu) ikiwa ni sawa na marejesho ya miezi mitatu ya mwaka wa kwanza wa uwekezaji. Dhamana hii itatumika muda wote wa mkataba.
- ii. Mwajiri atalazimika kutumia dhamana ya uwekezaji pale ambapo mwekezaji atashindwa kulipa kiasi cha fedha alichohadi kurejesha Halmashauri ya Jiji la Mbeya.
- iii. Kutakuwa na nyongeza ya 3.5% ya gharama ya mkataba kwa kila mwaka ambapo Mwekezaji atatakiwa kumlipa mwajiri marejesho ya kila mwezi kwa mchanganuo ufuatao;
 - a) Mwaka wa kwanza =Tsh.4,000,000 (1+3.5%)⁰ =Tsh. 4,000,000.00 kila mwezi
 - b) Mwaka wa pili = Tsh.4,000,000 (1+3.5%)¹=Tsh. 4,140,000.00 kila mwezi
 - c) Mwaka wa tatu = Tsh.4,000,000 (1+3.5%)² =Tsh. 4,284,900.00 kila mwezi
 - d) Mwaka wa nne = Tsh.4,000,000 (1+3.5%)³ =Tsh. 4,434,871.50 kila mwezi
 - e) Mwaka wa tano = Tsh.4,000,000 (1+3.5%)⁴ =Tsh. 4,590,092.00 kila mwezi
 - f) Mwaka wa sita =Tsh.4,000,000 (1+3.5%)⁵ = Tsh. 4,750,745.22 kila mwezi
 - g) Mwaka wa saba =Tsh.4,000,000 (1+3.5%)⁶ =Tsh. 4,917,021.31 kila mwezi
 - h) Mwaka wa nane =Tsh.4,000,000 (1+3.5%)⁷ = Tsh.5,089,117.05 kila mwezi
 - i) Mwaka wa tisa =Tsh.4,000,000 (1+3.5%)⁸ = Tsh. 5,267,236.15 kila mwezi
 - j) Mwaka wa kumi =Tsh.4,000,000 (1+3.5%)⁹ = Tsh. 5,451,589.41 kila mwezi
- iv. Mkataba hautakuwa na mabadiliko tofauti ya bei zilizotajwa

5. MAPITIO YA MKATABA

Mkataba huu utakuwa na mapitio "contract review" kila baada ya miaka mitatu (3) juu ya uendeshaji wa mradi.

6. TARATIBU ZA UENDESHAJI NA UWEKEZAJI

Mwekezaji atatakiwa kuwasilisha kwa mwajiri taarifa ya ujenzi wa miundombinu kama ilivyowasilishwa kwenye andiko la mradi. Mabadiliko yoyote ya uwekezaji hayataruhusiwa hadi kibali cha mwajiri.

7. MAJUKUMU YA MWEKEZAJI

Katika mkataba huu mwekezaji atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo;

- i. Mwekezaji atatakiwa kujenga miundombinu yote ya mradi kwa gharama zake kama ilivyosanifiwa na kuwasilishwa kwa mwajiri. Pia atawajibika kusimamia na kuendesha shughuli zote za mradi kwa gharama zake
- ii. Mwekezaji atalipia gharama zote za uwekezaji na uendeshaji katika muda wote wa mkataba.
- iii. Mwekezaji atawajibika kutumia mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa Serikali kwa ujumla (GePG).
- iv. Mwekezaji atatakiwa kulipa kodi zote zinazotakiwa kulipwa kwa Halmashauri na Serikali kwa ujumla.

- v. Mwekezaji atatakiwa kukabidhi miundombinu na mali za mradi zikiwa kwenye ubora na kufanya kazi na kwamba umiliki utakuwa wa Halmashauri baada ya muda wa mkataba kumalizika. Aidha Mwekezaji atakuwa na haki ya kuomba kuendelea kuendesha mradi kama mpangaji baada ya muda wa mkataba huu kumalizika.
- vi. Mwekezaji atamkinga mwajiri dhidi ya hasara au uharibifu wa upande wa tatu ambapo atamkinga kikamilifu mwajiri wake dhidi ya madeni na hasara zinazotokana na Sheria ya ajira na fidia ya wafanyakazi na kwamba Halmashauri ya Jiji haitahusika na hasara yoyote itakayotokana na mwenendo wa uwekezaji.
- vii. Mwekezaji atatakiwa kutunza mazingira katika eneo la mradi kwa kuzingatia mahitaji na kanuni zote za mazingira kama zinavyoelekezwa na Serikali ya Tanzania.
- viii. Kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu za uwekezaji ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- ix. Kulipa kodi ya mwezi kwa kiwango kilichoainishwa katika mkataba huu.

8. MAJUKUMU YA MWAJIRI

Katika mkataba huu mwajiri atakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo;

- i. Kumsaidia na kumjengea mwekezaji mazingira rafiki ili afanye uwekezaji wake vizuri.
- ii. Kufanya ukaguzi na kufuatilia mwenendo wa mwekezaji katika utekelezaji wa mkataba huu.
- iii. Kumchukulia hatua za kisheria mwekezaji pindi atakapobainika kufanya uharibifu wa aina yoyote.
- iv. Kumiliki eneo la mradi kiwanja namba 31 kitalu G lililopo kata ya Sisimba mtaa wa Sokoine Mbeya mjini.
- v. Kumiliki miundombinu yote itakayokabidhiwa na mwekezaji baada ya kuisha kwa mkataba huu.

9. UTARATIBU WA KUSITISHA MKATABA

Upande wowote utakuwa na haki ya kuvunja mkataba baada ya kutoa notisi ya maandishi ya siku thelathini (30) kwa upande wa pili.

10. NJIA YA USULUHISHI WA MIGOGORO

Iwapo utatokea mgogoro baina ya pande mbili za mkataba huu, basi mgogoro huo utatatuliwa kwa njia ya majadiliano na majadiliano yakishindikana basi mgogoro huo utawasilishwa Mahakamani.

11. MAWASILIANO

Mawasiliano au maelekezo yoyote yanayohusiana na mkataba huu yatafanyika kwa lugha ya Kiswahili na kwa anuani zilizotajwa katika mkataba huu.

12. SHERIA ZITAKAZOTUMIKA KATIKA MKATABA

Mkataba huu utalindwa na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria Ndogo za mwajiri.

13. MIUNDOMBINU YA UWEKEZAJI

- (i) Mwekezaji atawekeza kwenye miundombinu ifuatayo;
- a) Mgahawa
 - b) Kilabu cha pombe
 - c) Ukumbi wa mikutano na sherehe
 - d) Eneo la kuoshea magari
 - e) Bwawa la kuogelea
 - f) Vyoo vya kulipia
 - g) Ofisi
 - h) Majengo ya maduka
 - i) Saloon ya kike na kiume
 - j) Bwawa la samaki

(ii) * Miundo mbinu inayotakiwa kujengwa ndani ya Bustani ni miundo mbinu inayohamishika na sio ya kudumu.

14. NYARAKA/VIAMBATISHO VYA MKATABA

Mkataba huu utasomwa pamoja na viambatisho vifuatavyo;

- i. Barua ya kutunuku zabuni
- ii. Andiko la biashara/Mradi
- iii. Muhtasari wa majadiliano
- iv. Nyaraka nyingine zinazohusu mradi
- v. Risiti ya malipo ya fedha ya dhamana ya uwekezaji

HIVYO BASI PANDE ZOTE ZINARIDHIA NA KUKUBALI KUFUNGWA NA MASHARTI YA MAKUBALIANO YA MKATABA, NA ZINAWEKA SAINI ZAO MBELE YA MASHAHIDI Kama ifuatavyo;

1. UPANDE WA MWAJIRI

Mkurugenzi wa Jiji
Jina. Amede A.E, Ng'wanidako

Mstahiki Meya wa jiji
Jina. Dormohamed Issa Rahmat

Saini
S.L.P 149 Mbeya
Namba ya Simu. 0767-581088
Tarehe. 21/05/2021

Saini
S.L.P 149 Mbeya
Namba ya simu. 076704153
Tarehe. 21/05/2021

2. UPANDE WA MWEKEZAJI;

Jina. BENSON S. MBEYA
Saini
Mtaa anaoshi. UZUNIQUMIA
Anuani. BOX 1688 - MBEYA
Namba ya simu. 0756 143624 / 0684 400004
Tarehe. 21/05/2021

Shahidi wa Mwekezaji
Jina. GIVEN ONIA NGASILO
Saini
Mtaa anaoshi. MATHOROFANI
Anuani. BOX 6 MBEYA
Namba ya simu. 0754 598919 / 0767 598919
Tarehe. 21/05/2021





JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI MBEYA



34

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na MCC/PMU/T.30/V.XIV/34

02/03/2021

Mkurugenzi,
Babito Trading Company Limited,
S.L.P 1688,
MBEYA.

YAH: KUKUTUNUKU ZABUNI NA: LGA/069/2020-2021/NCT/NCS/05 KWA AJILI YA UWEKEZAJI NA UENDESHAJI WA ENEO LA BUSTANI YA JIJI "CITY PARK".

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu,

2 Rejea zabuni yako iliyowasilishwa tarehe 27/11/2020 kwa katibu wa bodi ya zabuni Halmashauri ya Jiji Mbeya kwa ajili ya zabuni tajwa hapo juu na katika kikao cha bodi ya zabuni cha tarehe 17/01/2021 ulipitishwa na kupewa kazi hiyo ya uwekezaji na uendeshaji wa eneo la bustani ya Jiji "City Park" katika Halmashauri ya Jiji Mbeya.

3 Napenda kukujulisha kuwa umeshinda zabuni namba LGA/069/2020-2021/NCT/NCS/05 kwa ajili ya uwekezaji wa eneo bustani ya Jiji "City Park" kwa kipindi cha miaka kumi (10) kwa gharama zifuatazo;


- (i) Mwaka wa kwanza = $4,000,000.00(1+3.5\%)^0 = 4,000,000$ kwa kila mwezi
- (ii) Mwaka wa pili = $4,000,000.00(1+3.5\%)^1 = 4,140,000.00$ kwa kila mwezi
- (iii) Mwaka wa tatu = $4,000,000.00(1+3.5\%)^2 = 4,284,900.00$ kwa kila mwezi
- (iv) Mwaka wa nne = $4,000,000.00(1+3.5\%)^3 = 4,434,871.50$ kwa kila mwezi
- (v) Mwaka wa tano = $4,000,000.00(1+3.5\%)^4 = 4,590,092.00$ kwa kila mwezi
- (vi) Mwaka wa sita = $4,000,000.00(1+3.5\%)^5 = 4,750,745.22$ kwa kila mwezi
- (vii) Mwaka wa saba = $4,000,000.00(1+3.5\%)^6 = 4,917,021.31$ kwa kila mwezi
- (viii) Mwaka wa nane = $4,000,000.00(1+3.5\%)^7 = 5,089,117.05$ kwa kila mwezi
- (ix) Mwaka wa tisa = $4,000,000.00(1+3.5\%)^8 = 5,267,236.15$ kwa kila mwezi
- (x) Mwaka wa kumi = $4,000,000.00(1+3.5\%)^9 = 5,451,589.41$ kwa kila mwezi

4 Unapewa kipindi cha maandalizi cha miezi sita (6) kitachohesabiwa kuanzia tarehe ya mkataba

5 Utatakiwa kulipa fedha taslimu kiasi cha Tsh. 12,000,000/= (Milioni kumi na mbili tu) ikiwa ni dhamana ya utendaji kabla ya kusaini mkataba na kuanza kazi. Aina nyingine ya dhamana haitapokelewa.

6 Unatakiwa kujibu barua hii ya kuwa unakubali au unakataa kazi hiyo ndani ya siku tatu (03) kuanzia tarehe ya barua hii. Mkataba wa kazi utasainiwa baada ya kutekeleza maelekezo yaliyopo kwenye barua hii.

7. Nakutakia utekelezaji mwema,


Amede A.E. Ng'wanidako, MKURUGENZI WA JIJI
MKURUGENZI WA JIJI HALMASHAURI
HALMASHAURI YA JIJI MBEYA

TAARIFA YA KIKAO CHA MAJADILIANO NA MAKUBALIANO KUHUSU
UWEKEZAJI KATIKA ENEO LA MBEYA CITY PARK LINALOMILIKIWA NA
HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYAKILICHOFANYIKA TAREHE 21/01/2021

UTANGULIZI

Mnamo tarehe 18/02/2021 Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya aliteua timu ya wataalam watatu (3) kufanya majadiliano na mwekezaji aliyependekezwa kuhusiana na uwekezaji wa eneo la bustani ya Jiji (City Park). Wajumbe wa timu hiyo walikuwa wafuatao;

1. Edom Mrumah
2. Tekele.D. Makongo
3. Eng. Yunus Nsegobya


Timu ya majadiliano iliyoundwa na Mkurugenzi ilikaa na mwekezaji aliyepitishwa na Bodi mara baada ya kufanyiwa tathimini (evaluation) kupitia maombi ya "Tender No. LGA/069/2020-2021/NCS/PC/05" na kuonekana kukidhi vigezo. Mwekezaji aliyekabidhiwa kwa majadiliano ni BABITO TRADING COMPANY LIMITED.

HADIDU ZA REJEA (TOR)

Mambo sita (6) ambayo Bodi ilielekeza kwa Timu iliyoteuliwa ikiwa ni msingi wa mjadala utakaofanyika ni kama ifuatavyo:-






- (i) Kuongeza malipo ya kila mwezi kutoka kiasi cha Tshs. 3,000,000/= kufikia Tshs. 5,000,000/= kama bei ya kuanzia kabla ya majadiliano "To increase monthly payment".
- (ii) Bodi ilipendekeza kiasi cha asilimia 5% kitakuwa kikiongezeka kila mwaka wa mkataba. "Annual increment of monthly payment".
- (iii) Kufanya majadiliano kuhusu muda wa uwekezaji wa miaka 15 ambao mwekezaji alikuwa anaomba, bodi ilitoa mapendekezo ya miaka nane (8) hadi kumi kama msingi. (10) "To discuss issues related to Investment duration of 15 years".
- (iv) Kuweka dhamana ya uwekezaji "Performance bond" ya kiasi sawa na miezi mitatu (3)
- (v) Bodi pia ilipendekeza muda wa umiliki mali zisizohamishika kuwa miaka nane (8), pindi mwekezaji atakapo kuwa amezijenga na kumaliza mkataba wake. Baada ya muda huo mali hizo zitakuwa zinamilikiwa na Halmashauri ya Jiji. "Infrastructures ownership after lapse of contract".
- (vi) Bodi ilipendekeza kipindi cha miezi sita (6) kama muda wa malazamio na baada ya hapo mwekezaji atapaswa kuanza kulipa miezi mitatu kwanza kabla ya kuanza. "Grace period".

Maandalizi ya kikao cha kamati ya majadiliano yalifanywa chini ya Mwenyekiti wa timu ndugu, Edom Mrumah ambaye alifanya mawasiliano na mwekezaji na kukubaliana kukutana tarehe 21/01/2021 katika Ofisi za Halmashauri ya Jiji, kitengo cha manunuzi chumba namba 107.



UTAMBULISHO

Tarehe 21/01/2021 kikao cha majadiliano kilifanyika kuanzia majira ya saa 7:20mchana kwa kuhusisha timu toka Halmashauri ya Jiji na mwekezaji ambaye ni Mkurugezi wa BABITO TRADING COMPANY LIMITED pamoja na Mkaguzi wake wa Hesabu (Internal Auditor). Orodha ya majina ya waliohudhuria ni kama ifuatavyo:-

NA.	JINA	CHEO	SIFA	SAINI
1.	Edom Mrumah	Mchumi	Mwenyekiti	
2.	Tekele .D. Makongo	Mhasibu	Katibu	
3.	Yunus Nsegobya	Mhandisi	Mjumbe	
4.	Benson J. Mrema	Mkurugenzi Babito	Mjumbe	
5.	Nicholas Thadei Kiria	Mkaguzi wa ndani Babito	Mjumbe	

Baada ya utambulisho huo, mwenyekiti wa kikao alimshukuru na kumpongeza mwekezaji kwa moyo wa uzalendo na ubunifu alioonyesha kama mzawa wa kuwekeza katika nchi yake na hususani katika Jiji la Mbeya na endapo uwekezaji huu, utaratibiwa vizuri kama ulivyo kwenye "business plan" basi mradi unanafasi kubwa sana ya kulibadilisha Jiji la Mbeya kwa kuwa na eneo nzuri la mapunziko na biashara kwa ujumla. Mwenyekiti wa kikao alitoa nafasi kwa mwekezaji endapo ana neno kabla ya mjadala, mwekezaji aliomba mwenyekiti tufungue kikao kwa sala na kishakuendelea na ajenda za kikao, na baada ya sala kikao kilifunguliwa na kuwakaribisha wajumbe na mwekezaji katika kikao.

MAJADILIANO NA MAKUBALIANO

1. Mada ya kwanza ni juu ya malipo ya kila mwezi, ambayo mwekezaji aliomba kulipa kila mwezi kiasi cha Tzs.3,000,000/= kupitia "Tender document"na bodi ilipendekeza kiasi cha TZS. 5,000,000/= Lakini majadiliano ya swala hili ilikuwa kama ifuatavyo, Mkurugenzi wa Babito alielezea ni kwa nini anahitaji malipo ya Tzs. 3,000,000/= ni kutokana na fursa zitakazojitokeza kwa upande wa Halmashauri ya Jiji kuchaji vitu vingine kama vile leseni za biashara na ushuru wa huduma, hofu juu ya wanasiasa kubadilikabadilika na maamuzi yao na jambo lingine ni marejesho ya mkopo benki pamoja na riba yake, kwani uwekezaji huu utahitajika fedha zingine zikopwe benki ili kuweza kufanikisha uwekezaji kama nilivyoomba. Timu iliyoundwa ilitafakari jambo ilo kupitia "business plan" na kufanya tathimini ya faida itakayokuwa anapata mwekezaji kwa mwezi na mwaka pindi mradi utakapo kuwa umekamilika.Baada ya majadiliano, wajumbe walikubaliana kuwa mwekezaji ailipe Halmashauri kiasi cha Tzs. 4,000,000/= kwa mwezi.
2. Mada ya pili ni pendekezo la asilimia 5% kiasi ambacho kitakuwa kikiongezeka kila mwaka wa mkataba na kulipwa kila mwezi (Annual increment of monthly payment) ambacho kilipendekezwa na bodi. Mwekezaji aliomba alipe kiasi cha asilimia 2.5% kisha kupanda hadi asilimia 3%, sababu kubwa ya mwekezaji kuomba hivyo ni kutokana na ajira nyingi atakazo toa kwa wazawa, ambao pia watahitaji kulipwa

aliwaeleza wajumbe baada ya kupitia kitabu cha zabuni na "business plan" na kufanya hesabu wamejiridhisha kuwa mwekezaji kwa kipindi cha kufikia mlaka kumi (10) anaweza kabisa kurudisha gharama za uwekezaji na kupata faida. Mkurugenzi wa Babito Trading Co. Ltd alikubali mkataba wa uwekezaji kwa miaka kumi (10), isipokuwa aliomba ofisi ya Halmashauri impatie mkataba ambao utakuwa na mapitio "Renewable contract" ili kumpa nafasi ya kuendelea kuboresha mazingira ya biashara yatakayotokana na wahitaji au wateja "customers" katika muda wa uwekezaji. Baada ya mjadala wajumbe wamekubaliana muda wa mkataba utakuwa miaka 10 (kumi).

4. Mada ya nne ilihusu muda wa uwekezaji wa miaka 15 ambao mwekezaji alikuwa anaomba, bodi ilitoa mapendekezo ya miaka nane (8) hadi kumi (10) kama msingi. Baada ya mwekezaji kuja na wazo jipya la kupewa miaka thelethini (30) timu ya majadiliano baada ya kushindwa kufikia makubaliano ili omba kuhairishwa mjadala huo, ili iweze kupata mawazo mapana kuto ngazi za juu kabla kufikia maamuzi. Mwekezaji alilidhia ombi la kuahirisha kikao siku hiyo ya tarehe 21/01/2021 majira ya saa 11:24 Jioni hadi tarehe 29/01/2021 saa 5:30 Asubuhi.
5. Mada ya tano ni kipindi cha miezi sita (6) kilichopendekezwa na bodi kama muda wa matazamio (Grace period) na baada ya hapo mwekezaji atapaswa kuanza kulipa miezi mitatu kwanza kabla ya kuanza. Mwekezaji alikuja na ombi la kuongezewa muda kufikia mwaka moja badala ya miezi sita, baada ya maelekezo ndugu; Tekele Makongoalimwelekeza mwekezaji kuwa katika kiwango cha serikali za mitaa haturuhusiwi kuwa na muda wa matazamio unaozidi mwaka mmoja labda kuanzia ngazi za wizara, hivyo kufanya miezi sita kwa kiwango cha Halmashauri ni sahihi kabisa. Mwekezaji alikubaliana na kulizika na maelezo yaliyotolewa, hivyo wajumbe wa majadiliano kwa pamoja wamekubaliana kipindi cha miezi sita (6) kiwe ndicho kipindi cha matazamio (Grace period) na kufanya malipo ya miezi mitatu (3) kabla kuanza biashara.

BAADA YA KUAHIRISHA KIKAO

Timu ilitoa taarifa ya kuhairisha kikao kwa mkuu wa idara ya manunuzi ndugu, BOSCO KOMBA ili aweze kuwasilisha swala hilo kwa Mkurugenzi wa Jiji. Baada ya kuwasilisha swala hilo Mkurugenzi alilipokea na kuwaita baadhi ya wakuu wa Idara na timu tarehe 22/01/2021 majira ya saa 10:08 Jioni kwa ajili ya kujadili, katika kikao hicho cha dharura wajumbe walioshiriki ni wafuatao:-

mishahara mizuri na pia ulipaji wa kodi ya mapato. Swala la kodi ya mapato ndugu Edom Mrumah alimweleza mwekezaji kuwa Serikali imekuwa ikitoa muda wa matazamia pindi mwekezaji anapoanza kuwekeza ili kumwezesha kusimama au kuinuka vizuri kibiashara na kupata uelewa mpana juu ya mzunguko wa biashara hususani katika mapato. Timu ilipendekeza tena asilimia 4.5% kulingana na mtuliliko wa faida ulivyoonyeshwa kwenye "business plan" kuwa mwekezaji atakuwa anapata faida kila mwezi na kila mwaka. Mwekezaji alieleza kuwa kutokana na baadhi ya gharama zingine kulipwa mapema mara tu baada ya miezi sita (6) kumalizika kama kipindi cha matazamia na wakati huo ametoka kuwekeza kwenye miundo mbinu na muda wa kujenga miundo mbinu ni mchache kutokana na makubaliano, hivyo mwekezaji aliomba iwe asilimia 3.5% kwa kuzingatia sababu zilizotolewa hapo juu. Timu pamoja na mwekezaji baada ya mjadala mpana, pande zote walikubaliana iwe asilimia 3.5% kama nyongeza ya marejesho kwa miaka inayoendelea ya uwekezaji baada ya mwaka wa kwanza.

Timu ilifanya mchanganuo wa kihesabu wa "Annual rate of return" ili kujilizisha kabla ya kufanya maamuzi, timu ilitumia kanuni ya kihesabu ilikufikia maridhiano; $P(1+r\%)^n$

Kama inavyoonyesha hapo chini:-

- (i) Mwaka wa kwanza = $4,000,000.00(1+3.5\%)^0 = 4,000,000$
- (ii) Mwaka wa pili = $4,000,000 (1+ 3.5\%)^1 = 4,140,000.00$
- (iii) Mwaka wa tatu = $4,000,000 (1+ 3.5\%)^2 = 4,284,900.00$
- (iv) Mwaka wa nne = $4,000,000(1+ 3.5\%)^3 = 4,434,871.50$
- (v) Mwaka wa tano = $4,000,000(1+3.5\%)^4 = 4,590,092.00$
- (vi) Mwaka wa sita = $4,000,000(1+ 3.5\%)^5 = 4,750,745.22$
- (vii) Mwaka wa saba = $4,000,000(1+3.5\%)^6 = 4,917,021.31$
- (viii) Mwaka wa nane = $4,000,000(1+3.5\%)^7 = 5,089,117.05$
- (ix) Mwaka wa tisa = $4,000,000(1+3.5\%)^8 = 5,267,236.15$
- (x) Mwaka wa kumi = $4,000,000(1+ 3.5\%)^9 = 5,451,589.41$

Kutokana na mchanganuo hapo juu Halmashauri ya Jiji kwa kipindi cha miaka kumi itapata ongezeko la TZS. 1,451,589.41 ambalo ni sawa na ongezeko la 36.29%.

3. Mada ya tatu ilikuwa ni juu ya muda au kipindi cha uwekezaji (Investment duration). mwekezaji aliomba apewe miaka 30 (Thelathini) kutokana na majengo mengine atakayo jenga kuwa ya kudumu, jambo ambalo hakulielezea kwenye kitabu chake alichoombea zabuni "Tender document" na bodi ilipendekeza miaka nane (8) hadi kumi (10). Hivyo baada ya mjadala mrefu, mjumbe wa timu ndugu; Tekele Makongo aliwaeleza wajumbe kuwa ili kuharakisha utekelezaji na uwajibikaji ni vizuri kipindi kisiwe kirefu sana, sambamba na kuangalia muda sahihi ambao mwekezaji anaweza kurudisha gharama zake na kuanza kupata faida. Ndugu Edom Mrumah

**ORODHA YA MAJINA YA WALIOHUDHURIA KIKAO CHA DHARURA TAREHE
22/01/2021**

NA.	JINA	CHEO	SIFA
1.	Amede E.A. Ng'wanidako	Mkurugenzi Jiji	Mwenyekiti
2.	Tekele D. Makongo	Mhasibu	Katibu
3.	Triphonia Kisiga	Mwanasheria Jiji	Mjumbe
4.	Kimolo Mikina	Afisa Tehama Jiji	Mjumbe
5.	Bosco Komba	Afisa Ugavi Jiji	Mjumbe
6.	Edom Mrumah	Mchumi	M/kiti wa timu

Katika kikao hicho kilianza kwa katibu wa timu ndugu; Tekele Makongo kutoa taarifa fupi ya mjadala ulipofikia, wajumbe wa kikao walikubaliana na mambo manne tuliyokwisha kukubaliana katika mjadala. Kuhusu swala la umiliki wa miundo mbinu ya kudumu "Infrastructure ownership" mara baada ya mkataba kwisha, mapendekezo ya wajumbe wa kikao cha dharura mara baada ya mjadala mpana, wajumbe walikubaliana iwe miaka kumi (10) kama mwisho wa umiliki miundo mbinu ya kudumu zitakazowekwa na mwekezaji na kisha mali hizo kumilikiwa na Halmashauri ya Jiji na endapo mwekezaji atahitaji kuendelea basi atapangishwa kama mpangaji katika majengo hayo na sio mmiliki tena.

Kikao pia kiliona umuhimu wa kuongeza nguvu kwa kumteua ndugu; MASHAKA SEMKIWA ambaye ni Mkuu wa kitengo cha ukaguzi wa ndani wa jiji (Internal Auditor) ili kuongeza nguvu katika timu, kuhusiana na swala hilo la miundo mbinu ya kudumu pindi mkataba utakapo kwisha.


Baada ya makubaliano Mkurugenzi aliangiza timu ya majadiliano kuendelea na mjadala na makubaliano kwa kuangalia masilahi mapana ya Halmashauri ya Jiji na endapo kutakuwa na kutokuelewana basi timu isisite tena kutoa taarifa ili kupata muafaka sahihi. Hivyo mwenyekiti wa timu alifanya mawasiliano na mwekezaji ambaye ni Mkurugenzi wa BABITO TRADING CO.LTD kumtaarifu juu ya kuendelea na mjadala kwa mada iliyosalia ya umiliki wa miundo mbinu mara baada ya muda wa mkataba kwisha, mwekezaji aliomba tukutane tarehe 29/01/2021. Mwenyekiti alikubaliana na ombi lake na kumuomba afike majira ya saa 5:30 Asubuhi.

MENGINEYO:

Mwenyekiti aliomba ajenda hii ifanyike haraka kulingana na jambo jinsi lilivyo, hususani namna ya kumpata mwekezaji kutoka Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

KUFUNGA KIKAO:

Mwenyekiti aliahirisha kikao na kuwatakia wajumbe utekelezaji mwema wa majukumu.



.....
JINA: - EDM MRUMAH
MWENYEKITI








.....
JINA: - TEKELE D. MAKONGO
KATIBU

.....
17/02/2021
TAREHE

TAARIFA YA KIKAO CHA MAJADILIANO NA MAKUBALIANO KUHUSU UWEKEZAJI KATIKA ENEO LA MBEYA CITY PARK LINALOMILIKIWA NA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA KILICHOFANYIKA TAREHE 29/02/2021

UFUNGUZI WA KIKAO:

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kikao cha pili mara baada ya kuahirishwa. Mwendelezo wa kikao cha mjadala kilianza kwa sala majira ya saa 6:09mchana siku ya tarehe 29/01/2021 chini ya mwenyekiti ndugu; Mashaka Semkiwa, ambaye alimshukuru mwekezaji na kuelezea umuhimu wa kuendelea na mjadala hususani kwenye eneo la umiliki wa miundo mbinu (Infrastructure Ownership). Mwenyekiti pia alimwomba radhi mwekezaji kwa usumbufu uliojitokeza wa kuahirisha mjadala ili kupata uelewa wa pamoja kwa maslai ya pande zote mbili. Waliohudhuria katika kikao ni kama ifuatavyo:-

NA.	JINA	CHEO	SIFA	SAINI
1.	Mashaka Semkiwa	Mkaguzi wa ndani Jiji	Mwenyekiti	
2.	Tekele D. Makongo	Mhasibu	Katibu	
3.	Yunus Nsegobya	Mhandisi	Mjumbe	
4.	Benson J. Mrema	Mkurugenzi wa Babito	Mjumbe	
5.	Nicholas Thadei Kiria	Mkaguzi wa ndani wa Babito	Mjumbe	

Mwenyekiti wa timu ndugu, Mashaka Semkiwa aliwaeleza wawekezaji kama tumekubaliana muda wa mkataba kuwa miaka kumi (10) kwa nini muda wa umiliki wa miundo mbinu pia usiwe miaka kumi (10). Babito alieleza kuwa swala la kuomba muda wa miaka 25 kwa miundo mbinu ya kudumu waliliangalia katika mtazamo wa kiuchumi kutokana na hali ya Dunia ilivyo sasa.

Mkaguzi wa Jiji aliwaeleza pia mikataba mingi ya Halmashauri ya Jiji inaanzia miaka mitano (5) hadi (8) lakini ninyi mna bahati kuwaruhusu kuwekeza kwa miaka kumi (10) tofauti na wengine, hivyo tumetoa kipaumbele kwenu.

Mhandisi aliwaeleza wawekezaji kuhusiana na barua walioandika inayoelezea uwekezaji hauitakuwa wa kudumu, lakini ramani inaonyesha kutakuwa na majengo ya kudumu mbali na yale ya nje. Babito hatuta jenga majengo ya kudumu maeneo ya ndani, isipokuwa tutaweka vitu ambavyo ni rahisi kuviondoa na maeneo ya kuzunguka nje ndiko tutajenga majengo ya kudumu.

Pia mkaguzi wa ndani alihoji kupitia "Business plan" ambayo haionyeshi gharama ya vitu vinavyoonyeshwa kwenye mchoro wa ramani. Michanganuo midogomidogo ilikuwa ni muhimu ili kuthibitisha usahihi wa gharama iliyo kwenye "Tender Document", hivyo kama mnaweza kutenganisha gharama ili kurahisisha usimamizi ni muhimu kuendelea kuboresha gharama hizo.

Mkurugenzi wa Babito Trading Co. Ltd alikubaliana na swala hilo licha ya kuwa gharama hizo zilijumuishwa kwenye "Business plan" hivyo aliahidi kulifanyia kazi na siku ya jumatatu tarehe 01/02/2021 atawasilisha mchanganuo wa gharama hizo dogodogo.

MATOKEO YA MJADALA BAADA YA KUAHIRISHA

Mwisho kikao kwa pamoja kilikubaliana kuwa kipindi cha umiliki wa miundo mbinu mara baada ya mkataba kwisha utakuwa miaka kumi (10), lakini pindi mkataba unapoisha kipaumbele cha kuongeza mkataba kiwe kwa mwekezaji aliyopo sasa, kwa kuzingatia makubaliano ya mchakato mzima wa uwekezaji huu, ambao unampatia nafasi na uwezo mwekezaji kuongeza mkataba husika kwa kushirikisha pande zote mbili toka kwa mwekezaji na Halmashauri ya jiji. Pia mwekezaji aliomba kipengele cha miundo mbinu ya kudumu kiingizwe kwenye mkataba ili kuondoa mwingiliano wa kisiasa pindi inapotokea mabadiliko ya kisiasa.

Mwekezaji pia aliomba apewe miezi mitatu kuanzia sasa ili kuanza maandalizi ya kuweka vitu.

Mkaguzi wa ndani wa jiji alimweleza mwekezaji kuwa miezi mitatu ni sawa, japo kuwa anaweza kuanza na kutengeneza mazingira ya ndani ambayo hayana matumizi yoyote mpaka sasa ili kuepuka kutumia muda mrefu.


MENGINEYO:

Mwekezaji BABITO TRADING CO. LTD alikubaliana na wazo hilo la kuanzia ukarabati ndani ya eneo ambalo hakuna shughuli zozote zinazo endelea kwa sasa (eneo la ndani)na yuko tayari kuanza mara baada ya mkataba kukamilika.

KUFUNGA KIKAO:

Mwenyekiti alifunga kikao cha majadiliano mara baada ya kupata ombi kutoka kwa Mkurugenzi wa Babito majira ya saa 07:18 Mchana na kuwaomba walengwa kuendela kuwasiliana endapo kunasababu za kufanya hivyo.

Naomba kuwasilisha,


.....
JINA: - MASHAKA SEMKIWA
MWENYEKITI


.....
JINA: - TEKELE D. MAKONGO
KATIBU

17/02/2001
.....
TAREHE



MBEYA CITY GARDEN BUSINESS PLAN

(Proposed for BBQ & Restaurant, Bar/Lounge, Venue-Hall/Tent, Car Washing-Parking & Commuter Services, Line of a Modern City Shops, Hair & Beauty Salon-Gents/Ladies, Swimming Pool, Fish Pond, Public Toilets, Office, Kids Games -Jumping castles,)

TABLE OF CONTENTS

1.0 Business/Executive Summary	4
Business Objectives	6
Mission Statement	6
Guiding Principles/Values Statements	6
1.1 Keys to Success	8
2.0 Company Description	8
Ownership	8
Legal Form	8
Start-Up Summary	9
Location and Facilities	9
3.0 Products	9
Products/Services Descriptions	9
Competitive Comparison	9
Inventory Management	9
Future Products/Services	10
4.0 Market Analysis	10
Industry Analysis	10
4.1.1 Market Size	10
4.1.2 Industry Participants	10
4.1.3 Main Competitors	11
4.1.4 Market Segments	11
Market Tests	11
Target Market Segment Strategy	12
4.1.5 Market Trends	12
4.1.6 Market Growth	12
Positioning	13
5.0 Marketing Strategy and Implementation	13
SWOT Analysis	13
5.1.1 Strengths	13
5.1.2 Weaknesses	13
5.1.3 Opportunities	14
5.1.4 Threats	14
Strategy Pyramid	14
Competitive Edge	14
Marketing Strategy and Positioning	15
5.1.5 Positioning Statement	16
5.1.6 Pricing Strategy	16
5.1.7 Promotion and Advertising Strategy	16
5.1.8 Website	17
5.1.9 Marketing Programs	17



MBEYA CITY GARDEN BUSINESS PLAN

(Proposed for BBQ & Restaurant, Bar/Lounge, Venue-Hall/Tent, Car Washing-Parking & Commuter Services, Line of a Modern City Shops, Hair & Beauty Salon-Gents/Ladies, Swimming Pool, Fish Pond, Public Toilets, Office, Kids Games -Jumping castles.)

Sales Strategy	17
5.1.10 Sales Programs	18
Legal	18
Exit Strategy	18
6.0 Organization and Management	18
Organizational Structure	18
Management Team	19
7.0 Financial Plan	19
Important Assumptions	19
Start-Up Costs (See attachment Annex I)	19
7.1.1 Projected Cash Flow (See attachment Annex II)	20
7.1.2 Projected income/Profit and Loss (see attachment Annex III)	20
7.1.3 Working Capital (see attachment Annex IV)	20
7.1.4 Projected Balance Sheet (see attachment Annex V)	20



MBEYA CITY GARDEN BUSINESS PLAN

(Proposed for BBQ & Restaurant, Bar/Lounge, Venue-Hall/Tent, Car Washing-Parking & Commuter Services, Line of a Modern City Shops, Hair & Beauty Salon-Gents/Ladies, Swimming Pool, Fish Pond, Public Toilets, Office, Kids Games -Jumping castles.)

1.0 Business/Executive Summary

Mbeya is becoming a more attractive city with diverse business activities particularly hotel, restaurant, venues, food and drink cultures, Car washing and commuter services, Hair and beauty salon (gents and ladies), recreation and fitness centre (swimming pool), Fish pond, public toilets, office, kids games (Jumping castles). The growing number of the above so stipulated justifies the general likeness of people living here.

However, the Babito Trading Co Ltd observed that there is something is still missing in organizing what will fit the needs of Mbeya residents and non residents. Babito Trading Co Ltd after get on hold of this tender will not just put something on place without add any value of it, incessantly maintain its value of which will not only create a centre of attection to locals but also to the foreigners and fill at home. The idea of opening MBEYA CITY GARDEN offering the above services was emerged from this gap of quality and endearing service.

The MBEYA CITY GARDEN will be a unique gathering place in Mbeya Region. By providing exemplary service and will be the premier mode in Mbeya. As a growing city, Babito though of this services need to be facilitated here in the City.

We plan to supply services and products that enhance our clients' physical appearance and mental relaxation. Hair and beauty salon will unleash the needs of those who are in stress to be taken care of by proving a relaxing environment with great customer service, we know People love to be taken care of, women love having great colored nails done and men love having perfect hands and beards, this facility will ensures there will be a well designed rooms for massaging powered on with a networked Television on board, soft drinks provided, all these will be well facilitated at MBEYA CITY GARDEN.

Swimming pool will be an added recreation and fitness centre that will suit the need for the guest during summer and other season throughout the year. This will foster the health status of the people around in Mbeya and give a new look for Mbeya City as a growing City equipped with services available in other region hence increase the chance for more people come and invest here in souththen highland. We have looked at what sort of pool complex is needed in Mbeya. So we have proposed a enlargement of the facilities once leased that area, a wrap around building which will provide an enlarged gym, a fitness studio, new changing rooms and entrance.

The facility of a swimming pool in Mbeya is needed for Health (aiding and improving the general health of the residents of Mbeya and its surrounding area), Education (the teaching of swimming skills, particularly to young people), Safety (improving individuals personal safety when near water by being able to swim and generally know how to handle themselves, know



MBEYA CITY GARDEN BUSINESS PLAN

(Proposed for BBQ & Restaurant, Bar/Lounge, Venue-Hall/Tent, Car Washing-Parking & Commuter Services, Line of a Modern City Shops, Hair & Beauty Salon-Gents/Ladies, Swimming Pool, Fish Pond, Public Toilets, Office, Kids Games -Jumping castles,)

danger signs), Sport (provide a resource that can be used for water sports, events, teams, and related training), Pleasure (providing an all-age community facility that adds to the quality of life in the area, for family recreation, water fun parties), Social/Business Hub (to act as a core when providing other health/social facilities for example, beauty therapy, gymnasium dance studio, social/refreshment area personal fitness programmes (some of which could be under specialist trainer guidance)

The success of the Venue (Hall), Bar/Lounge) and Barbeque are in its owner – with collectively 10+ years experience in the hotel, conference, restaurant and bar industry. He is committed to making this operation a successful one. Employees have been hand selected and share the same views as the owner, that is, keeping the customer happy assures repeat business.

The MBEYA CITY GARDEN has plans to initially capture 2% market share by fiscal Year One, and an additional 3% and 5% for Years Two to Five respectively. The MBEYA CITY GARDEN will accomplish this through a concerted advertising and marketing campaign, reliance on signage and primarily by word of mouth. Located at a major intersection in Mbeya City centre.

The MBEYA CITY GARDEN is willing to lease such an area space in the city center for a period of five years and paying back all obligly dues as will be in a concerted agreement. Upon the lease acceptance Babito make an offer to pay that rental mothly payment of Tshs 3,000,000 million, basing on his projected cash flow. The MBEYA CITY GARDEN will be owned and operated by Babito Trading Co Ltd

The Babito Trading Co Ltd is interested to acquire the tender advertised located in Mbeya city. The location has never been utilized for the so mentioned purpose and therefore veneue(hall/Tent) building facility, lavatories, furnitures, fixtures and equipment need to be installed instantly upon acquire this tender.

Sales projections annually is expected to be Tshs 915,904,962/= turnover, with 2%-5% growth rate in a year, which positions BABITO BABITO TRADING CO LTD as a highly desirable concept for Ownerhip in a table service market where is considered moderately profitable and therefore a good investment. Total start up costs will be roughly around Tshs 931,520,600/= of which will be contributed by the Owner with no secured bank loan will be needed.

[Signature]
27/11/2020

[Signature]
27/11/2020



MBEYA CITY GARDEN BUSINESS PLAN

(Proposed for BBQ & Restaurant, Bar/Lounge, Venue-Hall/Tent, Car Washing-Parking & Commuter Services, Line of a Modern City Shops, Hair & Beauty Salon-Gents/Ladies, Swimming Pool, Fish Pond, Public Toilets, Office, Kids Games -Jumping castles.)

Business Objectives

The MBEYA CITY GARDEN will be a newly established area accommodated with hall/tent, bar/lounge, barbeque restaurant and kids games in Mbeya. This business idea will cater to office workers and tourists during the day, wedding facility, kids jumping games and at night, the bar will cater to local customers coming home from work for some relaxation. The Garden will provide a top score menu featuring traditional bar fare along with fine food offerings. On weekends the MBEYA CITY GARDEN will feature live music band including a coustical guitar and small jazz venues.

The investment will accomplish these goals by holding itself apart from competition as a true neighborhood bar, offering a vast selection of beer and wine, by providing fine cuisine in addition to standard bar fare, all in a relaxing environment designed to make customers return.

Mission Statement

The MBEYA CITY GARDEN will provide a comfortable place for locals to come and gather for relaxation, wedding striving to be the venue, barbeque and bar of choice for the locals in Mbeya. The MBEYA CITY GARDEN is based on the guiding principles that life is to be enjoyed and this is reflected in its vast selection of beverages, its delicious food offerings and the professional team members.

Vision Statement

Adhering to the Babito Trading Co Ltd vision on:

- ✦ Providing the highest customer service to our internal and external customers
- ✦ Offering innovative ways of providing Hotel Industry & pharmaceutical and social care with knowledgeable and compassionate staff, and
- ✦ Continuing to grow and be profitable in an ever-changing hotel & health care environment.

Guiding Principles Values Statements

